# Mwanasheria

JARIDA LA AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

AGC ZANZIBAR | ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS




SCAN ME

TOLEO LA 005 JANUARI - JUNI 2026
Scan kusoma Jarida kielektroniki
www.agcz.go.tz

HALIUZWI

# SALAMU ZA MHE. MWANASHERIA MKUU



**Nachukua fursa hii kwa mara nyengine kuwakaribisha Wasomaji wetu katika Toleo la Tano la Jarida letu linaloandaliwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar.**

Kupitia kurasa za toleo hili, ninafuraha kuendelea kuwasilisha kwa Wananchi taarifa muhimu zinazoakisi shughuli mbali mbali zilizotekelezwa na Afisi katika kipindi kilichopita, zikionesha mshikamano, uwajibikaji na uadilifu wa kisheria.

Lengo kuu la kuchapishwa kwa Jarida la MWANASHERIA ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya mambo mbalimbali yanayowakabili hasa yale yanayohusu sheria.

Kwa kuzingatia kuwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ndio Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala ya kisheria, Toleo hili pamoja na mambo mengine linaendelea kuchukua juhudi mbali mbali zinazosaidia kuifanya kazi hiyo ya ushauri kwa ufanisi zaidi.

Moja ya habari kuu ni kikao cha ushirikiano baina ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Benki ya CRDB, ambacho kililenga kuimarisha mahusiano ya Taasisi na kuendeleza mashirikiano yenye tija kwa maendeleo ya Zanzibar.

Mashirikiano hayo ni kielelezo cha dhana ya kujenga mifumo thabiti ya kisheria na kifedha kwa manufaa ya Umma.

Aidha, kupitia Mashirikiano hayo, Afisi kwa kushirikiana na Benki hiyo iliendesha mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Taasisi nyingine za kiserikali yaliyolenga kuwajengea uelewa wa Sheria za kimataifa, Mikataba ya kifedha na mbinu za majadiliano wakati wa kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu Mikataba ya mikopo ili kulinda maslahi ya Umma.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu licha ya mafunzo hayo, pia imefanya mafunzo mengine ya ndani kwa Mawakili ambayo yalihusu eneo la Misamaha ya Kodi katika Mikataba.

Lengo la Afisi kujikita katika mafunzo hayo ni kuimarisha zaidi uelewa kwa Mawakili ili kutekeleza majukumu yao ya kutoa ushauri unaozingatia maslahi ya nchi wakati wa kupitia Mikataba hasa kipinidi hiki cha Awamu ya Nane.

Itakumbukwa kuwa, kipindi hiki cha Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais, Dkt. Hussein Ali Mwinyi lipo ongezeko kubwa la mahitaji ya rasilimali za kifedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Miradi hiyo ni kama Barabara, Bandari, Skuli, Viwanja vya Ndege na vituo vya afya ambayo chimbuko lake ni Mikataba inayopaswa kuwasilishwa na kutolewa ushauri katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa.

Aidha, imeandaliwa Makala kuhusu "Utaratibu wa Utwaaji wa Ardhi na vilivyoendelezwa" ya kuifahamaisha Jamii miongozo ya kisheria na kiutendaji kuhusu taratibu za utwaaji wa Ardhi ili kulinda haki za Wananchi na pia kusimamia maslahi mapana ya Taifa.

Ni vyema Wananchi wafahamu kuwa katika kipindi hiki ambacho miradi mingi ya maendeleo inatekelezwa hapa nchini, upo uwezekano mkubwa wa baadhi ya Wananchi kuchukuliwa Ardhi zao.

Hata hivyo, jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba, Serikali hulazimika kuchukua Ardhi hizo kwa kuzingatia maslahi ya Umma.

Katika ukurasa mwengine, lipo Shairi kuhusu umuhimu wa utunzaji wa miundombinu mbali mbali ya kimaendeleo ambayo imejengwa na inayoendelea kujengwa nchini.

Ni vyema kila Mwananchi kuchukua juhudi binafsi kuhakikisha kuwa miundombinu hiyo inadumu kwa kipindi kirefu ili kunufaisha kizazi cha sasa na kijacho.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu itaendelea kuwa nguzo muhimu ya uwajibikaji na ulinzi wa maslahi ya Umma kwa kuhakikisha sheria zinatungwa na kusimamiwa kwa uadilifu na kwa manufaa ya Wananchi wote.

Wito wangu kwa Wasomaji wa Jarida hili na Wananchi kwa ujumla, kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali ili iendelee kutimiza ahadi zake za kuwaletea maendeleo.

Kwa pamoja, tuendelee kulinda na kuimarisha misingi ya haki na utawala wa sheria Zanzibar.

**Dkt. Mwinyi Talib Haji,**
**Mwanasheria Mkuu,**
**Zanzibar.**

# TAHARIRI



**Kwa heshima na taadhima tuanze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha tena kukamilisha Jarida letu la MWANASHERIA.**

Baada ya shukran hizo, tuwakaribishe tena kwa moyo mkunjufu Wasomaji wetu kutenga muda wa kulisoma Toleo hili la Tano ambalo limesheheni Habari na Makala mbali mbali zinazolenga kuielimisha jamii katika masuala kadhaa hasa yanayohusu masuala ya kisheria.

Makala na Habari tulizoandaa tunaamini zinaweza kuwa msingi mzuri wa Watu katika jamii wanaokabiliwa na masuala ya kisheria kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili ambazo zinahitaji kufuata misingi ya sheria.

Jarida letu limekuwa daraja muhimu la kuwasilisha kwa Wananchi taarifa za kazi na majukumu ya Afisi ambayo ina jukumu la kusaidia Umma hasa katika kutoa ushauri wa kisheria.

Aidha, Jarida hili lina lengo la kuihamasisha jamii kufuata kikamilifu Sheria mbali mbali ili kuimarisha uwajibikaji, demokrasia na utawala bora hapa nchini.

Kwa muhtasari, katika toleo hili tumeandaa kwa Wasomaji wetu Habari za matukio kadhaa na Makala mbali mbali za kitaalamu ambazo zinaweza kuupatia Umma taaluma na maarifa.

Miongoni mwa habari zilizomo ni pamoja na Habari ya tukio la Kilele cha Wiki ya Sheria Zanzibar inayoonesha umuhimu wa matumizi ya mifumo ya kiteknolojia katika sekta ya sheria.

Habari kuhusu kikao cha ushirikiano na Benki ya CRDB pamoja na mafunzo yaliyowezeshwa na Benki hiyo kwa Mawakili wa Serikali, ni hatua inayojenga misingi ya mashirikiano ya kitaasisi kwa manufaa ya taifa.

Habari kuhusu kupandishwa Madaraja kwa Mawakili wa Serikali, ni ishara tosha ya kutambua juhudi na mchango wa Wanasheria wetu katika kulinda maslahi ya Umma na kusimamia haki.

Pia ipo habari inayohusu tukio la kuagwa kwa Katibu Muhtasi aliyestaafu Utumishi wa Umma katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu, habari ambayo inatufundisha thamani ya kujitolea na uaminifu wakati wote wa utumishi.

Habari ya Afisi kutoa elimu ya kisheria inadhihirisha dhamira yetu ya kuimarisha uelewa wa Wananchi juu ya haki na wajibu wao pamoja na kuiepusha jamii kujiingiza katika makosa yasiyo ya ulazima.

Aidha, Makala kuhusu "Utaratibu wa Utwaaji wa Ardhi na vilivyoendelezwa" ni Makala inayotoa mwongozo wa kisheria na kiutendaji kuhusu taratibu za utwaaji wa ardhi, ikilenga kulinda haki za wananchi na maslahi mapana ya taifa.

Makala ya "Ukomo wa Kesi za Madai" inatoa mwanga wa kitaalamu na kijamii juu ya masuala yanayogusa moja kwa moja maisha ya Wananchi na hatua stahiki za kuchukua kudai haki kabla ya muda wa kudai haki hizo kumalizika.

Vile vile, Makala kuhusu "Utaratibu wa kupata fao la kuumia kazini kutoka ZSSF" ni Makala inayoelimisha jamiii hasa Watumishi wa Umma na Taasisi binafsi kufahamu haki zao na kuzipigania kisheria.

Tunapenda pia kutambua na kushukuru maoni kutoka Taasisi mbali mbali na Wananchi ambao ndio wasomaji wetu yanayolenga katika kuliimarisha zaidi Jarida letu ambayo tumekuwa tukiyapokea na kuyafanyiakazi. Maoni hayo ni kioo cha matarajio na yanatupa muongozo wa kuimarisha zaidi utendaji wetu na Jarida letu.

Niwaombe wasomaji wetu wote na wadau kwa ujumla kulisoma Jarida letu tukiamini kwamba taaluma iliyomo inaweza kuwa na msaada mkubwa kwa Jamii yetu.

Shukrani za pekee ziende kwa wote waliowezesha maandalizi ya Jarida hili na tunahimiza wadau wote kuendelea kulisoma na kulitumia kama nyenzo ya kujifunza na kubadilishana mawazo.

Tunapenda wasomaji wetu kuendelea kushirikiana nasi kwa kutoa maoni na ushauri, ili kwa pamoja tuweze kujenga taifa lenye misingi imara ya haki na usawa.

**Shaaban R. Abdalla,**
**Mwenyekiti wa Bodi ya Wahariri.**


**BODI YA WAHARIRI**

**Mwenyekiti:**
Shaaban R. Abdalla
(Naibu Mwanasheria Mkuu)

**Wajumbe:**
Dkt. Abdul-Nasser H. Hikmany
Mdungi M. Mdungi
Salim M. Abdalla
Asya M. Ahmed
Shufaa A. Khamis
Nakhla A. Massoud
Abeid M. Saleh
Hamisa M. Makame
Faki H. Mjaka

**Msanifu:**
Kombo Z. Kombo (mzubeir)
**Mshauri:**
Ramadhan M. Suleiman

# Taasisi za Kisheria Zahimizwa Kutumia Mifumo ya Kielektroniki



Viongozi mbali mbali wakimsikiliza Mwanasheria Mkuu (hayupo pichani) wakati wa kutoa hotuba katika hafla ya kilele cha Wiki ya Sheria iliyofanyika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Wete Pemba.

**NA MWANDISHI WETU**

**SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua za kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi kwa Muhimili wa Mahkama ili kuzidisha uwajibikaji wa upatikanaji wa haki nchini.**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla alipomuwakilisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Sheria Zanzibar, hafla iliyofanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi uliopo Wete kisiwani Pemba.

Alisema katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imewekeza zaidi shilingi Bilioni 13.6 kwa ujenzi wa majengo ya kisasa ya Mahkama ambayo yanaendana na uwekaji wa miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi.

Aidha, Mhe. Hemed alifahamisha kuwa Serikali inaendelea kuwekeza katika matumizi ya TEHAMA kuelekea Serikali Mtandao, ili kutimiza azma ya kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbali mbali hasa katika matumizi ya mfumo wa usimamizi wa mashauri na mifumo mengine itakayozidisha uwajibikaji katika mchakato mzima wa upatikanaji wa haki.

Alisema kupitia mfumo huo usajili wa mashauri utakuwa rafiki, usikilizaji na uamuzi wa mashauri utafanyika kwa haraka sambamba na upatikanaji sahihi wa takwimu, kuongezeka kwa uwazi na kukuza uwajibikaji miongoni mwa wadau wa Sheria.


Kwa upande wake Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji akizungumzia kuhusu kauli mbiu ya maadhimisho hayo, isemayo "Maboresho ya Mfumo wa TEHAMA kwa Taasisi za Sheria", alisema Afisi ya Mwanasheria Mkuu imenunua vifaa vya mfumo wa kieletroniki kwa lengo la kurahisisha na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Afisi hiyo.

Alisema, kwa sasa Afisi ipo katika hatua za mwisho za kumpata Mshauri Elekezi atakayesimamia uandaaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu na kusimamia hatua muhimu za utekelezaji wa majukumu ya Afisi.

Dkt. Mwinyi alifahamisha kuwa, kwa hatua ya awali, mfumo huo utahusisha taarifa muhimu za Mawakili wa Serikali wanaofanya kazi au wanaosimamiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, pamoja na kuweka kumbukumbu za hatua mbali mbali zinazopitiwa katika mikataba ya Serikali na kazi nyengine zinazofanywa na Afisi.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla akihutubia kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, katika kilele cha Wiki ya Sheria iliyofanyika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Wete Pemba.



Katika hatua za kujiwekea taratibu za kazi zinazoeleweka na kutekelezeka kwa umakini na ufanisi, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeandaa Miongozo ya Kiutendaji (Manuals) na tayari Afisi imechapisha na kusambaza Muongozo wa Uandishi wa Sheria ambao unatoa maelezo na utaratibu mzima wa uandishi wa sheria na kanuni nchini.

Akitoa salamu za Mahkama Jaji Mkuu wa Zanzibar Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla alisema Matumizi ya TEHAMA yataleta mageuzi makubwa ya kiutendaji kwa kufanya kazi kwa ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika kufikia upatikanaji wa haki kwa wananchi.

Jaji Khamis alisema mifumo mitano imeundwa kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi wa mahkama ikiwemo mfumo wa usimamizi wa mashauri ambao utazifanya mahkama kuondokana na matumizi ya karatasi na mawakili watafungua mashauri ya kesi bila ya kufika mahakamani.

Jaji huyo aliitaja mifumo inayotumiwa na Mahkama za Zanzibar kuwa ni pamoja na mfumo wa usimamizi wa mashauri, Mfumo wa ZAN-WAKILI, Mfumo wa Tume ya Utumishi ya Mahkama, Mfumo wa Malalamiko na utoaji wa maoni pamoja na Mfumo wa Uhifadhi wa hukumu za Mahkama.

Nae Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mhe. Mwalim Dkt. Haroun Ali Suleiman amesema Wizara yake itaendelea kushirikiana na watendaji wa Mahkama katika kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira bora, wezeshi na salama hasa kutokana na umuhimu wa utendaji kazi wa Muhimili huo.

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji akizungumza katika hafla ya kilele cha Wiki ya Sheria iliyofanyika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Wete Pemba.

# Mawakili watakiwa kujiongeza kitaaluma kwenye mikataba, sheria za kimataifa




*Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla (wa pili kushoto), akitoa hotuba ya ufunguzi kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib kuhusu mafunzo ya Mikataba yaliyoandaliwa na Benki ya CRDB yaliyofanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Madinat Al Bahr, Mbweni Zanzibar.*

**MWANDISHI WETU**

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji, amewataka Mawakili wa Serikali kuwa na uelewa wa sheria za kimataifa, mikataba ya kifedha na mbinu za majadiliano wakati wa kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu mikataba ya mikopo ili kulinda maslahi ya Taifa.

Dkt. Mwinyi ametoa wito huo huko katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Mwanasheria Mkuu, Ndg. Shaaban Ramadhan Abdalla kwenye ufunguzi wa mafunzo yaliyoandaliwa na Benki ya CRDB, hafla iliyofanyika katika ukumbi wa hoteli ya Madinat el Bahr.

Alisema tofauti na mikopo ya masharti nafuu, mikopo ya kibiashara huja na vigezo na viwango vya kibiashara vinavyoendana na soko, masharti ya ulipaji yenye ukomo na uwajibikaji mkubwa na mara nyingi huambatana na masharti ya kisheria yenye uzito mkubwa.

Alitahadharisha kuwa, mikopo hiyo huhitaji umakini wa hali ya juu katika maandalizi, majadiliano na utekelezaji wake.

"Lengo ni kuhakikisha kuwa Serikali haiingii katika mikataba itakayosababisha kudumaza uchumi wa nchi kwa muda mrefu", alisema Dkt. Mwinyi.

Alibainisha katika awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuna ongezeko la mahitaji ya rasilimali za kifedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa barabara, bandari, viwanja vya ndege na vituo vya afya.

Alisema ili kukabiliana na mahitaji ya kifedha, Serikali imekuwa ikitumia mbinu za upatikanaji wa fedha, ikiwemo utaratibu wa kupata mikopo ya kibiashara.

Alieleza kuwa mikataba ya aina hiyo mara nyingi huandaliwa kwa kufuata viwango vya kimataifa na hujumuisha vipengele muhimu ikiwemo sheria itakayotumika, utaratibu wa utatuzi wa migogoro hususan kupitia usuluhishi wa kimataifa, dhamana za Serikali na mgawanyo wa hatari kati ya wahusika wa mkataba.

"Kutokana na upekee huo, ni dhahiri kwamba mawakili wa Serikali wanapaswa kuwa na uelewa mpana wa sheria za kimataifa, mikataba ya kifedha, pamoja na mbinu za majadiliano kwa ajili ya kulinda maslahi ya taifa katika mikataba hii", alisema Dkt. Mwinyi.

Alisisitiza kuwa, utaratibiwa kupata mikopo unahusisha mikataba mikubwa baina ya Serikali na wakopeshaji.

Hali hiyo inaweka wajibu mkubwa kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na mawakili wa Serikali kwa ujumla, kuhakikisha mikataba yote inafanyiwa uchambuzi wa kina wa kisheria kabla ya kutiwa saini kwa ajili ya utekelezaji wake.

Kadhalika, alisema mawakili wa Serikali wanatakiwa kuhakikisha maslahi ya Serikali yanalindwa kikamilifu, kuhakikisha kuwa masharti ya mikataba ni ya haki, wazi na yanayotekelezeka na hatari zote zinazoweza kujitokeza zinatambuliwa mapema na kudhibitiwa ipasavyo.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Sheria kutoka CRDB, Pascal Mihayo, alisema wamekuwa wakifanya miradi mikubwa kwa ushirikino na serikali kufanikisha mikopo hiyo.

"Tumekuwa tukifanya mikopo hii na Serikali chini ya Mwanasheria Mkuu, lakini kutokana na uzoefu wa muda mrefu, kwa hiyo tumeona ni vyema kuweka mafunzo na majadiliano namna tunavyoweza kusaidiana katika kuingia mikataba", alisema Mihayo.

Alieleza katika mafunzo hayo wameangalia mambo muhimu ya kufanyika kabla, wakati na baada ya kuingia mikataba ili kukwepa mitego inayoweza kuhatarisha maslahi ya umma katika mikataba hiyo.

Alisema awali mikataba ilikuwa inaweza kuchukua hadi miezi sita mpaka kukamilika lakini baada ya mafunzo hayo wanatarajia itafupishwa muda ili Serikali ipate fedha haraka kwa ajili ya maendeleo.

Alieleza kuwa mikataba ambayo ni dhaifu Serikali inaweza kupata hasara kwani umuhimu wa mkataba ni kuuangalia kabla ya kuingia kwani inatakiwa kuhakikisha wanalinda maslahi yao.

Naye, Meneja wa CRDB Tawi la Zanzibar, Fatma Nassor alisema watafungua fursa nyingi kwani mambo ya sheria yakiwa sawa hata biashara zao zitazidi kuimarika.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Rasilimali Watu, Utawala na Mipango kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Dkt. Abdul-Nasser H. Hikmany alisema katika awamu hii ya nane, Serikali imekuwa ikiingia katika mikataba inayochochea maendeleo, hivyo mafunzo hayo yatawajengea uelewa mkubwa ili kusaidia kuitolea ushauri mikataba inayokuja katika Afisi yao.

Naye Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Ushauri, Ndg. Latifa Suleiman, alisema kabla ya kuingiwa kwa mikataba, kuna haja ya wanasheria kuifahamu vyema mikataba hiyo kila kipengele ili wasaidie kutoa ushauri wa kitaalamu utakaosaidia kuifanya mikataba hiyo kuwa na tija kwa wananchi na taifa kwa ujumla.



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya Mikataba yaliyoandaliwa na Benki ya CRDB kwa Mawakili wa Serikali wakifuatilia mafunzo. Hafla hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Madinat Al Bahr, Mbweni Zanzibar.*

## Makala maalum

# Utwaaji wa Ardhi na vilivyoendelezwa kwa Maslahi ya Umma



*Mradi wa Nyumba za kisasa uliopo Kisakasaka, Mkoa wa Mjini Magharibi unaotekelezwa na Shirika la Nyumba (ZHC) ambao ni matokeo ya wananchi kutoa maeneo ya ardhi kwa ajili ya kupisha miradi ya kimaendeleo.*

**NA ALI HAMAD - AGC**

UTWAAJI wa ardhi ni uwezo wa Serikali kuchukua haki binafsi katika ardhi kwa maslahi ya umma. Sheria za Zanzibar zinatambua fursa kwa wananchi kumiliki ardhi kwa mtu ambaye ana haki au ya maslahi ya haki ya umiliki binafsi.

Makala hii inaeleza kuhusu taratibu za ulipaji fidia kwa wananchi pale haki yake ya matumizi ya ardhi inapochukuliwa na Serikali. Miongoni mwa taratibu hizo za ulipaji fidia zimeelezwa katika Katiba, Sera na Sheria zifuatazo:

Katiba ya Zanzibar ya 1984: Katiba imeeleza kuwa mali ya mtu yeyote isichukuliwe kwa nguvu bila ya kulipa maslahi au haki yoyote inayotokana na mali hiyo bila ya kutimizwa masharti yaliyoelezwa na Katiba.

Masharti hayo ya Katiba yanajumuisha, kuwe na umuhimu wa kuchukuliwa kwa mali hiyo (mfano ulinzi, usalama, afya na upangaji wa mji), kulipa fidia kwa thamani ya soko iliyo haki, na kuwe kuna umuhimu mkubwa sana wa kuchukuliwa mali hiyo.

Sera ya Taifa ya Ardhi ya Zanzibar 2018: Sera ya Ardhi inatambua ardhi kuwa ina thamani, kiasi ya kuwekwa msingi wa ardhi hiyo kulipwa fidia stahiki na sahihi, ikiwa Serikali inataka kuitwaa ardhi kwa maslahi ya umma.

Sheria ya Umiliki wa Ardhi Nambari 12 ya 1992: Kwa ujumla wake, Sheria hii imekataza mtu kukatishwa haki ya umiliki wake wa ardhi, isipokuwa Waziri anaweza kusitisha haki yoyote ya umiliki kwa misingi ya maslahi ya taifa na kwa kulipa fidia.

Ingawa katika masuala yanayohusiana na umiliki wa ardhi katika Sheria hii, ardhi itakayochokuliwa au kukatishwa matumizi yake na Serikali kwa maslahi ya kitaifa, hayatalipwa kwa thamani ya soko isipokuwa kwa kile kilichoendelezwa juu ya ardhi ndio kitakacholipwa kwa thamani, kama ambavyo itaamuliwa wakati ambao amri ya ukatishaji wa matumizi hayo itakapotolewa.

Lakini kwa umiliki ambao unafuata

sheria nyengine, kama vile sheria ya Uhaulishaji Mali Sura ya 150 (1917), Sheria ya Utwaaji Ardhi Sura 95 (1909), Sheria ya Utwaaji Ardhi na Ukokotoaji Fidia Sura ya 96 (1949), inapaswa kulipwa kwa thamani halisi ya ardhi na kilichoendelezwa.


Sheria ya Utwaaji Ardhi Sura 95 (1909) , ingawa Sheria hii imepitwa na muda, haijafutwa na kwa kiasi kikubwa haitekelezwi, lakini ni muhimu kwani imeeleza kwa upana sana juu ya utwaaji wa ardhi.

Kwa namna yoyote itakayohitajika katika eneo lolote la ardhi kutumiwa na Serikali kwa maslahi ya umma ni vyema utaratibu wa kutwaa ardhi hiyo ufuatwe.

Taratibu hizo zinajumuisha utoaji wa taarifa kwa uwazi kabisa, ushirikishwaji wa wananchi, upimaji wa ardhi, uwekaji wa mipaka na alama katika eneo linalohitajika.

Sheria ya Utwaaji Ardhi na Ukokotoaji Fidia Sura ya 96 (1949): Kama ilivyo kwa Sheria ya Utwaaji Ardhi, Sheria hii nayo imebaki kuwa haitekelezwi kwa kiasi kikubwa kutokana na kupitwa na muda.

Hata hivyo, Sheria hii haijafutwa na ni vizuri kuitolea maelezo kwani imeweka utaratibu wa namna ya kutoa maamuzi ya kiwango cha fidia kinacholipwa kwa ajili ya ardhi inayochukuliwa kwa maslahi ya umma.



*Muonekano wa Barabara ya juu (Flyover) Mwanakwerekwe, katika Mkoa wa Mjini Magharibi, ambao ni matokeo ya wananchi kutoa maeneo ya ardhi baada ya kulipwa fidia ili kupisha miradi ya kimaendeleo.*

Malipo hayo yatafanywa kwa kuwekwa mazingatio ya thamani ya ardhi (market value for land). Fidia inajumuisha pia thamani ya malipo ya hasara yoyote iliyojitokeza katika ardhi wakati wa kutwaa, mazingira yatakayomlazimu mtu kubadilisha makaazi yake, au hasara yoyote ambayo itaonekanwa kwa nia njema mtu kuhitajika kulipwa faida ya ardhi kutokana na kuchukuliwa umiliki wake, pamoja na kuzingatia kiwango cha malipo ya ziada ya asilimia kumi na tano (15%).



*Muonekano wa Mradi wa Nyumba za kisasa huko Kisakasaka, Mkoa wa Mjini Magharibi utakavyokuwa baada ya kukamilika, kutokana na wananchi kutoa maeneo yao kupisha miradi ya kimaendeleo.*

Kwa kuzingatia misingi hiyo ya Kisera, Kikatiba na Kisheria, ni dhahiri kuwa utwaaji wa ardhi Zanzibar unapaswa kuwa mchakato wa wazi unaozingatia ushirikishwaji wa dhati wa wananchi na haki ya mmiliki kupata fidia kamili.

Utekelezaji huo utasaidia kulinda haki za raia, kuchochea maendeleo yenye usawa, na kupunguza au kuondoa kabisa migogoro isiyo ya lazima baina ya wananchi na Serikali.

Aidha, ni vyema wananchi wafahamu kuwa wakati Serikali inapotwaa ardhi inafanya hivyo kwa maslahi ya taifa.

Kwa mfano miradi ya kimaendeleo inayoendelea kwa sasa nchini ikiwemo miundombinu ya barabara, hospitali, viwanja vya ndege na skuli inathibitisha dhamira ya dhati ya jambo hilo.

# Mawakili wa Serikali wapigwa msasa wa kusimamia Mikataba



*Dkt. Michael J. Marere kutoka Taasisi ya Ushauri ya Loreme Consulting Group (LCG), akitoa mafunzo kwa mawakili wa Serikali yaliyohusu Misamaha ya Kodi katika Mikataba. Hafla hiyo imefanyika Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Mazizini Zanzibar.*

**NA MWANDISHI WETU**

NAIBU Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Ndg. Shaaban amesema Serikali kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu inatumia gharama kutafuta wataalamu wa ndani na nje ya Zanzibar wa masuala ya Mikataba wanaoweza kutoa mafunzo kwa mawakili wa serikali yatakayowasaidia kuimarisha utendaji kazi zao.

Naibu Shaaban amesema hayo wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa mawakili wa Serikali yaliyohusu Misamaha ya Kodi katika Mikataba na kuongeza kuwa mafunzo hayo yanalenga kuongeza umahiri wa Mawakili katika kusimamia na kutekeleza mikataba kwa ufanisi.

Alisema, ana imani kuwa wataalamu hao watakidhi mahitaji na hivyo kusaidia kuongeza weledi kwa mawakili hao ili kulinda maslahi ya serikali na wananchi kwa ujumla.

Alisema malengo ya mafunzo hayo si tu kuwasaidia mawakili, bali kuisaidia nchi kwa ujumla hasa ikizingatiwa kuwa, serikali ya awamu nane imejikitaka kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alibainisha kuwa nchi inahitaji kufaidika kwa kupata kodi kupitia mikataba ambayo serikali inaingia, hivyo ni vyema mawakili wakafahamu masuala ya kodi na misamaha yake ili watoe ushauri mzuri wakati wa kupitia mikataba hiyo.

Naibu Shaaban aliongeza kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kuimarisha taasisi zake na kuandaa wataalamu wenye uwezo wa kushughulikia changamoto za kisheria zinazojitokeza katika sekta mbalimbali.

Akizungumza katika mafunzo hayo mkufunzi, Dkt. Michael J. Marere kutoka Taasisi ya Ushauri ya Loreme (LCG) alisema, kumekuwa



*Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar Ndg. Shaaban R.*
*wa Serikali yaliyohusu Misamaha ya Kodi.*

na ombwe katika uandaaji wa mikataba na kwamba Serikali inaingia katika miradi mingi ya kimaendeleo ambapo pamoja na mambo mengine inahitaji kupata misamaha.

Dkt. Marere amesema, kazi iliyonayo Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni kuhakikisha misamaha ya kodi inaendana na sheria hiyo na kwamba hilo ndio ombwe lenyewe.

Alisema ni jukumu la watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kujua sheria za kodi hasa kwenye maeneo yanayohusu misamaha ya kodi ambayo haiendani na sheria.

Aliishauri Afisi kuendelea kutoa mafunzo mbali mbali kuhusiana na sheria za kodi hasa maeneo ya misamaha ikiwemo misamaha kwenye sheria za kodi za kimataifa ili Afisi hiyo iendelee kutoa ushauri unaozingatia maslahi ya nchi.

Kwa upande wake Mkuu wa Divisheni ya Usimamizi wa Mikataba kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Ndg. Abeid Saleh, alieleza kuwa, mikataba ni nyenzo muhimu ya kisheria inayohitaji uangalizi wa karibu ili kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na ulinzi wa maslahi ya taifa.

Naye Mkuu wa Divisheni ya Uhusiano wa Kikanda na Kimataifa kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Ndg. Chai Ali Mohamed, alieleza kuwa, hatua hiyo ni ya kupongezwa kwani itawasaidia wafanyakazi kuboresha utendaji wao wa kazi na kuongeza ufanisi katika kusimamia mikataba ya Serikali.

Wakati huo huo, Wakili wa Serikali Yakub Rajab aliishukuru Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuandaa mafunzo hayo ya kuimarisha uwezo wao wa kitaalamu, hususan katika kipindi ambacho Zanzibar inashuhudia ongezeko la miradi mingi ya maendeleo na uwekezaji.



*Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar Ndg. Shaaban R. Abdalla (kulia), akifungua mafunzo kwa mawakili wa Serikali yaliyohusu Misamaha ya Kodi katika Mikataba.*



*Abdalla (katikati) akiwa na washiriki wa mafunzo ya siku mbili kwa mawakili*

# Ufahamu Ukomo wa Madai kisheria



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali na Wananchi wakibadilishana mawazo katika ukumbi wa Mahkama kabla ya kuanza  kusikilizwa kwa Mashauri ya Madai, Kisiwani Pemba.*

**NA SAFIA SULTAN-AGC**

UKOMO wa madai ni moja ya misingi muhimu katika Sheria za Madai, ambapo dhana hii inaweka mipaka ya muda ambao ndani yake muhusika/mdai anapaswa kuwasilisha madai yake Mahkamani.

Lengo la kuwekwa kwa ukomo wa madai ni kuhakikisha kwamba madai yanawasilishwa kwa wakati Mahkamani ili kuweza kupatikana haki.

Pia kuona kwamba madai yanafikia mwisho maana milango ya madai haiwezi kufunguliwa milele. Makala hii inatoa ufafanuzi wa ukomo wa ufunguaji wa kesi za madai.

**Dhana ya ukomo wa madai**

Dhana hii kwa Zanzibar inasimamiwa na Sheria ya Ukomo Sura ya 12 ya mwaka 1917 (Limitation Decree Cap 12 of 1917). Ukomo wa madai kisheria ni muda maalum uliowekwa na sheria ambao ndani yake mtu anaweza kufungua kesi mahkamani kudai haki.

Muda huo maalum uliowekwa ukimalizika pasipokuwa na sababu zinazokubalika kisheria, mtu hawezi tena kufungua kesi na anazuilika kisheria kwa sababu muda wa kudai haki yake umemalizika (time barred).

**Madai na ukomo wake**

Kwa mujibu wa Sheria ya Ukomo Sura ya 12 ya mwaka 1917 (Limitation Decree Cap 12 of 1917), muda wa ukomo hutofautiana kulingana na aina za madai kwa mujibu wa Jadweli maalum lililopo katika Sheria hiyo.

| Aina ya Dai | Muda wa Ukomo |
|---|---|
| Migogoro ya Ardhi (Kurejeshewa ardhi) | Miaka 12 |
| Mikataba Iliyoandikwa na Kusajiliwa | Miaka 6 |
| Mikataba ya Kawaida/Deni la Pesa/Kodi | Miaka 3 |
| Uvunjaji wa Mkataba (Specific Performance) | Miaka 3 |
| Mishahara ya Wafanyakazi | Mwaka 1 |
| Kashfa (Libel/Slander) na Mashitaka ya Ovu | Mwaka 1 |
| Madai yenye msingi wa kisheria ya madhara | Miaka 3 |
| Jeraha la Mwili au Kufungwa Isivyo Halali | Mwaka 1 |

**Muda wa kipindi cha Ukomo wa Madai kuanza kuhesabiwa**

Muda huanza kuhesabiwa pale tu sababu ya msingi ya kudai (cause of action) inapojitokeza. Kwa mfano, siku mkataba unapovunjwa au siku mtu anapovamiwa kwenye ardhi yake.

**Kuhusu mazingira ya kusimama kwa muda**, Sheria inatambua kuwa kuna nyakati mtu hawezi kufungua kesi. Muda unaweza kusitishwa ikiwa kuna:

**Kizuizi cha Kisheria:** Mdai ni mtoto (chini ya miaka 18) au ana ugonjwa wa akili. Muda utaanza kuhesabiwa atakapofikisha umri wa utu uzima au kupata akili timamu;

**Udanganyifu (fraud):** Ikiwa mdaiwa alificha ukweli au nyaraka kwa hila, muda utaanza kuhesabiwa pale mdai atakapogundua udanganyifu huo; au

**Mdaiwa kuwa nje ya Nchi:** Muda ambao mdaiwa yuko nje ya Zanzibar hautahesabiwa katika kipindi cha ukomo.

**Ukomo wa Madai katika migogoro ya ardhi**, hapa ipo dhana ya **Umiliki wa Kutwalia (Adverse Possession).** Ikiwa mmiliki halali atakaa kimya kwa zaidi ya **miaka 12** bila kuchukua hatua dhidi ya mvamizi aliyeendeleza eneo hilo, anaweza kupoteza haki ya kumtoa mvamizi huyo. Mahkama Kuu ya Zanzibar imewahi kusisitiza kuwa sheria hii haina "huruma" kwa yule anayechelewa kudai chake.

Katika kesi ya ***DAVID ANNOSIS IBONDE v. MSELEM SHAZIL AME (Represented by his recognised agent Khamis Ame Khamis).*** Mahkma Kuu ya Zanzibar, Kesi ya Rufaa Nam.6 ya 2021. Mhe. Abdul-hakim A. Issa, J alieleza kwa tafsiri isiyo rasmi "kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika kifungu cha 4 mpaka 25 (vyote kwa pamoja),..

... kila shauri litakalofunguliwa baada ya kupita muda wa ukomo uliowekwa kwa mujibu wa Jadweli husika litafutwa, hata kama suala la ukomo halijawekwa kama utetezi katika shauri hilo", na shauri hili ilielezwa kwamba Mrufani/Mdaiwa alikuwa ni mvamizi wa ardhi lakini aliipata haki ya umiliki kwa kupita kwa muda wa miaka kumi na mbili (12).

Kwa ujumla, Sheria ya Ukomo wa madai ina nafasi muhimu katika mfumo wa haki kwa kuweka muda maalum wa kuanzisha madai Mahkamani kwani sheria inawasaidia wale wale walio macho na haki zao, na si wale wanaolala *(Equity aids the vigilant, not the indolent).*

Ukomo wa madai ni "upanga mkali" unaoweza kukata haki yako ikiwa hutaizingatia. Ni muhimu kwa kila mwananchi au mfanyabiashara kufuatilia madai yake mapema kabla muda haujapita (Time-Barred).

Ukishindwa kuzingatia muda huu, mahkama italazimika kuitupilia mbali kesi yako, hata kama una ushahidi wa wazi, kwani suala la ukomo ni la msingi kisheria.



*Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wakifurahia jambo kabla ya kuanza kwa Mashauri ya Kesi za Madai Mahkama Kuu Tunguu, Zanzibar.*

# Serikali yashinda kesi utaifishaji mali zilizohusisha mapato ya uhalifu



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali na Wananchi wakiwa katika Ukumbi wa Mahkama kabla ya kuanza kusikilizwa kwa Mashauri ya Madai, Mahkama Kuu, Tunguu.*

**NA MWANDISHI WETU**

AFISI ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar (ZDCEA), imepata ushindi katika Maombi ya Madai Na. 10 ya Mwaka 2024.

Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Kesi na Mashauri ya Madai katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Said Salim Said alisema kesi hiyo ilifunguliwa na Saleh Khamis Basleman na Gawar Bachi Fakir dhidi ya Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar.

Said, ambaye ni Wakili wa serikali Mkuu, alisema katika maombi hayo, waombaji waliiomba Mahkama Kuu Zanzibar kupitia upya uamuzi wa Kamishna wa ZDCEA wa Aprili 22 mwaka 2024, uliotangaza kutaifishwa kwa mali mbali mbali zikijumuisha nyumba na viwanja vilivyopo maeneo tofauti ya Zanzibar, kwa madai kuwa mali hizo zilipatikana kutokana na mapato ya uhalifu.

Aidha Mkurugenzi Said alifahamisha kuwa katika maombi yao, waombaji walidai kuwa hatua ya kutaifisha mali hizo ilikuwa kinyume cha sheria kwa kuwa ilifanyika bila ya amri ya Mahkama.

Hata hivyo, alisema baada ya kusikiliza hoja za pande zote, Mahkama imebaini kuwa Kamishna alitumia mamlaka aliyopewa kisheria chini ya Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti



*Baadhi ya Mawakili wa Serikali wakibadilishana mawazo baada ya kumalizika kwa Shauri la Madai, Mahkama Kuu, Tunguu.*

na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sheria Na. 8 ya Mwaka 2021.

Alifahamisha kuwa katika uamuzi alioutoa Juni 11 mwaka 2026, Mheshmiwa Jaji wa Mahkama Kuu H. S. Khamis (Tetere), alieleza kuwa waombaji hawakuweza kuthibitisha ukiukwaji wowote wa sheria au dosari za kiutaratibu ambazo zingehalalisha Mahkama kuingilia kati au kubatilisha uamuzi huo wa Kamishna.


Mkurugenzi huyo alifahamisha kuwa Mahkama iliridhika kuwa hoja za kisheria zilizowasilishwa na waombaji hazikuondoa wala kuathiri mamlaka ya Kamishna yaliyowekwa wazi na sheria husika.

Kutokana na sababu hizo, alisema Mahkama ilitupilia mbali maombi yote ya Waombaji na kuthibitisha uamuzi wa Kamishna wa Aprili 22 mwaka 2024 wa kutaifisha mali hizo kwa Serikali.

Uamuzi huo wa Mahkama ni miongoni mwa maamuzi ya mwanzo ya Mahkama Kuu ya Zanzibar, kuthibitisha na kuunga mkono mamlaka ya kisheria aliyopewa Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar ya kutaifisha mali zinazobainika kuwa zimetokana na mapato ya uhalifu, kwa mujibu wa Sheria Na. 8 ya Mwaka 2021.

Aidha uamuzi umekuja kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya na uhalifu wa kifedha, ili kuhakikisha kwamba mali zinazotokana na shughuli za uhalifu haziwanufaishi wahusika, bali zinarejeshwa kwa manufaa ya umma kwa mujibu wa Sheria.

# MATUKIO KA




Naibu Mwanasheria Mkuu, Ndg. Shaaban R. Abdalla (kulia), akionesha Muundo mpya wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu baada ya kuidhinishwa. Kushoto ni Katibu wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma Ndg. Kubingwa M. Simba.




Viongozi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wakiwa par
ikijumuisha Watoto Yatima.




Naibu Mwanasheria Mkuu Ndg. Shaaban R. Abdalla (kulia), akipokea seti ya jezi kutoka kwa Meneja wa Benki ya CRDB Tawi la Michenzani Mjini Zanzibar, Ahmad Aboubakar baada ya viongozi hao kumaliza mkutano wa ushirikiano wa taasisi zao.



Mkurugenzi Idara ya Mapitio na Utafiti wa Sheria
Abdul-Nasser Hikmany (katikati waliokaa) akiwa p
maoni kuhusu upandishaji wa madaraja na vyeo kw
Mjini Zanzibar.



Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba Mhe. Rashid Hadid Rashid akikagua Jarida la MWANASHERIA mara baada ya kukabidhiwa nakala ya Jarida hilo na Watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu baada ya kutembelea Banda la Afisi hiyo katika maonesho ya Wiki ya Sheria Gombani ya Kale, Chake Chake, Pemba.



Baadhi ya Wananchi wa Shehia ya M
mada zilizokuwa zikiwasilishwa na
walipofika katika Shehia hiyo kutoa el

# ATIKA PICHA



moja na washiriki wa Iftari iliyoandaliwa na Afisi hiyo



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji (wa pili kulia) akishiriki zoezi la kutoa sadaka kwa watoto yatima, baada ya kumaliza Futari iliyoandaliwa na Afisi yake.*



*kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Dkt. amoja na washiriki wa mkutano wa ukusanyaji wa va Watumishi wa Umma, hafla iliyofanyika Sebleni,*



*Mstaafu, Katibu Muhtasi Mwandamizi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Bi Khadija Ali Salum (wa pili kushoto) akiwa na baadhi ya wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu mara baada ya hafla ya kuagwa baada ya kustaafu Utumishi wa Umma.*



*lkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja, wakifuatilia Mawakili kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu, imu ya sheria kwa wananchi.*




*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC), Ndg. Sultan Said Suleiman akiwasilisha mada kuhusu Miradi ya Nyumba za kisasa kwa wafanyakazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuwashajiisha kununua nyumba hizo.*

# Mwanasheria Mkuu: Tutaendelea kupandisha madaraja Mawakili




*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji akitoa ufafanuzi kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika ukumbi wa Baraza hilo, Chukwani, Zanzibar.*

**NA MWANDISHI WETU**

MWANASHERIA Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji (AG), amesema Afisi yake imewapandisha madaraja Mawakili wa Serikali 58 kutoka wizara na taasisi mbali mbali, ili kuwawezesha kutekeleza vyema majukumu yao.

Mhe. Mwanasheria Mkuu alieleza hayo wakati akitoa ufafanuzi wa maswali mbali mbali yaliyoulizwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakati wa kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba na Sheria katika Mkutano wa Tatu wa Baraza la Kumi na Moja huko katika Ukumbi wa Baraza Chukwani, Zanzibar.

Dkt. Mwinyi aliahidi kuwa Afisi yake itaendelea kuwapandisha madaraja maafisa sheria wengine kulingana na mahitaji ili kuimarisha uwezo wa kitaaluma na maarifa katika majukumu yao ikiwemo ya kuitetea Serikali.

Alifahamisha kuwa kupitia kasi ya maendeleo yanayofanywa na Serikali na kazi ngumu zinazoendelea kufanywa, upo umuhimu wa kuwaongezea hadhi na majukumu Maafisa Sheria pamoja na Mawakili wa Serikali ambao wapo katika wizara na taasisi mbali mbali za umma.

"Hatuwezi kumpandisha daraja kila Wakili ama Afisa Sheria, katika kufanya hivyo ni lazima tuzingatie uwezo wake na mahitaji ya Serikali", alisema Mwanasheria Mkuu.

Dkt. Mwinyi alisema Serikali kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu itaendelea kuwajengea uwezo Maafisa sheria na Mawakili wake kwa kuwapa mafunzo ndani na nje ya nchi, sambamba na kuimarisha maslahi yao.

Alisema hatua hiyo husaidia kuimarisha uwezo wa Mawakili katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo




kuisimamia vyema Serikali katika kutatua kesi mbali mbali za madai, ushauri na usimamizi wa mikataba inayofikishwa kwenye taasisi waliopo.

Dkt. Mwinyi alifafanua kuwa tangu kuunganishwa kwa Tume ya Kurekebisha Sheria na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Sheria tisa zimefanyiwa mapitio, ambapo Sheria mbili zimeshawasilishwa katika sekta husika, huku Sheria mbili zikiwa katika hatua ya kupokea maoni kutoka kwa wadau.

"Nadharia ya Serikali kuijumuisha Tume ya Kurekebisha Sheria katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu, ni kuijengea uwezo zaidi na madhumuni yake ni kuonesha namna Tume hiyo inavyoendelea kutekeleza majukumu yake chini ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu", alifafanua.

Awali Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi akiwemo Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Mhe. Nadir Yussuf Al-wardy waliipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa namna inavyotoa ushauri wake wa kitaalamu juu ya Mikataba ya Serikali ambayo inaletwa katika Afisi hiyo.

Walisema licha ya Serikali ya Awamu ya Nane kuwa na ongezeko la mikataba mingi, Afisi hiyo inaendelea kujitahidi kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakati na kuirejesha mikataba hiyo kwa taasisi husika ili kufanyiwa kazi.

# Katibu Muhtasi Mwandamizi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu aagwa



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji akizungumza katika hafla ya kumuaga aliyekuwa Katibu Muhtasi Mwandamizi wa Afisi yake Bi Khadija Ali Salum baada ya kustaafu Utumishi wa Umma. Hafla ilifanyika katika Ukumbi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mazizini, Zanzibar.*



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji akiwa katika picha ya pamoja na Wafanyakazi katika hafla ya kumuaga aliyekuwa Katibu Muhtasi Mwandamizi wa Afisi yake Bi Khadija Ali Salum. Hafla hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mazizini, Zanzibar.*

**NA MWANDISHI WETU**

MWANASHERIA Mkuu wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi Talib Haji amempongeza aliyekuwa Katibu Muhtasi Mwandamizi wa Afisi yake, Bi. Khadija Ali Salum kwa kuonesha utiifu, uvumilivu na uzalendo katika utumishi hatua ambayo ilimuwezesha kuwa daraja la kusaidia watu wa ndani na nje ya Afisi hiyo.

Dkt. Mwinyi alitoa pongezi hizo katika hafla ya kumuaga Bi. Khadija baada ya kustaafu utumishi wa umma, hafla iliyofanyika ukumbi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mazizini, Zanizibar.

Alisema katika utumishi wake mtendaji huyo, alionesha mashirikiano kwa watu wa kawaida na viongozi mbali mbali, ambao kwa pamoja walisaidia kufanya kazi yake kwa urahisi hadi kufikia kustaafu utumishi wake kwa heshima.

Alifahamisha kuwa Bi. Khadija alikuwa Mwalimu wake wa kwanza mara baada ya kuteuliwa kushika wadhifa wake ambapo

alimsaidia kwa kumpatia miongozo mbali mbali na kwamba kama kuna mafanikio yaliyopatikana katika kazi zake, hivyo kuna mchango wa Bi. Khadija kutokana na kumsaidia katika kazi hizo.

Alimpongeza kwa kuanza kazi zake vizuri na kumaliza salama utumishi wake huku akimtakia kheri katika safari yake ya kustaafu.

Kwa upande wake Bi. Khadija akielezea historia yake ya utumishi, alisema alibahatika kufanya kazi zake vyema na viongozi mbali mbali ikiwemo marais wastaafu wa Zanzibar.

Katika utumishi wake, Bi. Khadija pia aliwahi kushiriki kazi mbalimbali ikiwemo Tume tofauti kama vile Tume ya kuchunguza Ajali ya Meli ya MV. Spice Islander, pamoja na Tume ya Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wake Naibu Mwanasheria Mkuu, Shaaban R. Abdalla akielezea historia ya kukutana na Bi. Khadija amesema wakiwa pamoja katika Tume ya kuchunguza ajali ya Mv. Spice Islander mwaka 2011, Naibu Mwanasheria Mkuu alivutiwa na utendaji kazi wake na kumuomba Mungu ajaalie kufanya kazi Afisi moja na Bi. Khadija jambo ambalo lilitimia baada ya kuteuliwa kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu mwaka 2020.

Naibu Shaaban alisema Bi. Khadija alikuwa Katibu Muhtasi mwenye weledi na mahiri, kwani alikuwa na uwezo mkubwa wa kutunza siri na kuandaa barua za kitaalamu bila shida yoyote.

Bi. Khadija katika utumishi wake alianza kuajiriwa serikalini mwaka 1982 na mwaka 2005 alianza rasmi kufanya kazi Afisi ya Mwanasheria Mkuu hadi kustaafu kwake.





*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji kulia akimkabidhi zawadi ya Jiko la kutumia umeme 'Oven' aliyekuwa Katibu Muhtasi Mwandamizi wa Afisi yake Bi Khadija Ali Salum baada ya kustaafu Utumishi wa Umma. Hafla hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Mazizini, Zanizibar.*



*Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Dkt. Mwinyi Talib Haji kushoto akimkabidhi zawadi ya Jokofu aliyekuwa Katibu Muhtasi Mwandamizi wa Afisi yake Bi Khadija Ali Salum baada ya kustaafu utumishi wa umma. Hafla hiyo ilifanyika katika Ukumbi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Mazizini Zanizibar.*

Makala maalum

# Namna ya watumishi wanavyoweza kupata fao la kuumia kazini kutoka ZSSF



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi (katikati) akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ZSSF Ndg. Nassor Shaaban Ameir kutokana na mchango wake muhimu kwa ZSSF, kulia ni Mke wa Rais, Mama Maryam Mwinyi.*

**NA MWANDISHI MAALUM ZSSF**

HIFADHI ya jamii ni dhana pana na kongwe inayotoa ufumbuzi wa matatizo ya kijamii na kiuchumi yanayoikumba jamii.

Hifadhi hiyo ni miongoni mwa nyenzo muhimu zinazomlinda mfanyakazi dhidi ya majanga mbalimbali au kwa upande mwengine inaweza kutafsiriwa kuwa ni mfumo wa kuendeleza kipato cha mfanyakazi pale ambapo kipato hicho kinapungua au kusimama kwa sababu mbali mbali.

Sababu hizo zinaweza kuwa uzee, ulemavu, ugonjwa wa kudumu, kuumia kazini, ukosefu wa ajira na majanga mengine yanayoweza kumpata mfanyakazi.

Kwa mujibu wa Ibara ya 25(1) ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 (Universal Declaration of Human Rights, 1948), hifadhi ya jamii ni haki ya msingi ya kila mwananchi duniani.

Aidha, utekelezaji wa tamko hilo uliendelezwa kupitia Azimio la Shirika la Kazi Duniani (ILO) kuhusu Viwango vya Chini vya Hifadhi ya Jamii, Namba 102 la mwaka 1952, ambapo ibara za 25, 53 na 59 zinaelezea juu ya haki ya wafanyakazi kupata hifadhi ya jamii.

Mbali na matamko na mikataba mbalimbali ya kimataifa, nchi nyingi duniani ikiwemo Zanzibar zimeendelea kuchukua hatua za kutunga sera, sheria na kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha wafanyakazi wanalindwa dhidi ya majanga mbalimbali, ikiwemo kuumia kazini wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kazi.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) umejikita katika utoaji wa Mafao mbali mbali, kwa lengo la kumlinda mfanyakazi dhidi ya majanga yanayoweza kumtokezea.

Mfano wa mafao hayo yanayotolewa hadi sasa ni:-

1. Fao la kuumia Kazini (Employment injury benefit)
2. Fao la Uzee (Old age benefit)
3. Fao la Ulemavu wa kudumu (Invalidity benefit)
4. Fao la Uzazi (Maternity benefit)
5. Fao la upotevu wa ajira (Unemployment benefit)
6. Fao la Urithi (Survival Benefit)

**Fao la kuumia kazini**

Kwa upande wa Zanzibar, msingi mkuu wa uwepo wa Fao la Kuumia Kazini (employment injury benefit), unatokana na Kifungu cha 10(g) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ambacho kinaeleza kuwa ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kuwa kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anapata fursa ya kufanya kazi, na msaada unatolewa kwa wasiokuwa na uwezo, wazee, wagonjwa, watoto na watu wenye ulemavu.

Aidha, msingi mwingine wa kisheria wa malipo ya Fao la Kuumia Kazini ni Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Namba 2 ya mwaka 2005, ambayo kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 5 ya mwaka 2022 iliongeza Fao la Kuumia Kazini kuwa miongoni mwa mafao sita yanayotolewa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF).

Katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na utaratibu endelevu na wenye ufanisi wa kulipa fao hili, Serikali kupitia ZSSF ilitunga Kanuni ya Fao la Kuumia Kazini ya mwaka 2023. Fao hili lilianza rasmi kulipwa tarehe 01 Julai 2023 kwa wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi walioumia kazini.

**Vigezo vya Kustahili Fao la Kuumia Kazini**

Fao la Kuumia Kazini hulipwa kwa wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi ambao ni wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF). Vigezo muhimu vinavyozingatiwa katika kulipa fao hili ni pamoja na:

1. Mfanyakazi kuumia akiwa kazini;
2. Mfanyakazi kufariki kutokana na ajali au mazingira ya kazi; na
3. Mfanyakazi kupata maradhi yatokanayo na kazi (Occupational Diseases).

Aina za Mafao ya Kuumia Kazini

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar hulipa mafao yafuatayo chini ya Fao la Kuumia Kazini:

1. Fao la Maumivu ya Muda;
2. Fao la Ulemavu wa Kudumu usiomzuia mfanyakazi kurejea kazini;
3. Fao la Ulemavu wa Kudumu unaomzuia mfanyakazi kurejea kazini;
4. Fao kwa mtu anayemhudumia mgonjwa asiyejiweza; na
5. Fao la Kifo.

**1. Fao la Maumivu ya Muda**

Fao hili hulipwa kwa mfanyakazi aliyepata maumivu kutokana na ajali au maradhi yatokanayo na kazi wakati au katika utekelezaji wa majukumu yake ya kazi.

Fao hili hukokotolewa kwa kuzingatia kiwango cha maumivu aliyopata mfanyakazi baada ya ajali au maradhi yanayotokana na kazi.

Kiwango cha fao ni sawa na nusu ya pato la siku la mfanyakazi likizidishwa kwa idadi ya siku ambazo mfanyakazi hakuhudhuria kazini kutokana na maumivu hayo.

Hata hivyo, fao hili halitalipwa iwapo mfanyakazi atakuwa amepewa muda wa mapumziko usiozidi siku tatu (3).

**2. Fao la Ulemavu wa Kudumu Usiozuia Kurudi Kazini**

Fao hili hulipwa kwa mfanyakazi aliyepata ajali au maradhi yatokanayo na kazi yaliyosababisha ulemavu wa kudumu lakini ambao haukumzuia kurejea kazini.

Fao hili hukokotolewa kwa kuzingatia asilimia ya ulemavu aliyopata mfanyakazi ikizidishwa na mshahara wa kima cha chini wa miezi 48.

**3. Fao la Ulemavu wa kudumu unaomzuia kurudi kazini**

Fao hili hulipwa kwa mfanyakazi aliyepata ajali au maradhi yatokanayo na kazi yaliyosababisha ulemavu wa kudumu ambao unamzuia kurejea kazini tena.

Fao hili hukokotolewa kwa kuzingatia asilimia ya ulemavu husika kwa msingi wa mshahara wa miezi 48.

**4. Fao kwa mtu anayemhudumia mgonjwa asiyejiweza**

Fao hili hulipwa kwa mtu wa karibu au mtu mwingine yeyote anayemhudumia mfanyakazi aliyepata ulemavu wa kudumu na ambaye hawezi kujihudumia kutokana na ajali au maradhi yatokanayo na kazi.

Kiwango cha fao hili ni robo ya kiwango cha fao la ulemavu wa kudumu alicholipwa mfanyakazi husika, na hulipwa kwa mkupuo mmoja.

**5. Fao la Kifo**

Fao la kifo hulipwa kwa wategemezi wa mfanyakazi aliyefariki akiwa kazini au kutokana na ajali au maradhi yatokanayo na kazi.

Fao hili hulipwa mara moja kwa mkupuo sawa na mshahara wa miezi 48 wa mfanyakazi aliyefariki.

Fao la kifo ni sehemu ya mali ya marehemu na hulipwa kwa warithi wake kupitia:

- Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar kwa mfanyakazi Muislamu; au
- Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara Zanzibar kwa mfanyakazi asiye Muislamu.

Utaratibu wa kuomba fao la kuumia kazini

Maombi ya fao la kuumia kazini yanaweza kufanywa na mfanyakazi mwenyewe au mtu mwingine kwa niaba yake kwa kumuandikia Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZSSF ndani ya kipindi cha wiki 12 tangu kutokea kwa ajali, kifo au kugundulika kwa maradhi yatokanayo na kazi.

Maombi hayo huwasilishwa kwa kujaza Fomu ya Maombi ya Fao (SSF 18) pamoja na kuambatisha nyaraka zifuatazo:

1. Nakala ya kadi ya uanachama wa ZSSF;
2. Cheti cha kifo (kwa madai ya kifo);
3. Taarifa ya daktari au matibabu;
4. Hati ya Polisi (PF3 au PF90);
5. Slipu ya mshahara;
6. "Sick sheet" au karatasi ya mapumziko ya matibabu;
7. Taarifa nyingine yoyote itakayohitajika; na
8. Taarifa ya Bodi ya Madaktari kwa mfanyakazi aliyepata ulemavu wa kudumu unaomzuia kurejea kazini.

Maombi hayatapokelewa wala kuzingatiwa iwapo yatawasilishwa nje ya muda wa wiki 12 tangu kutokea kwa tukio husika.

**Muda wa kulipa mafao**

Malipo ya fao la kuumia kazini hulipwa ndani ya siku 14 hadi 28 kulingana na aina ya maumivu au ukamilifu wa vielelezo vya madai viliyowasilishwa.

Mfumo wa malipo ya fao la kuumia kazini

Malipo ya fao la kuumia kazini hufanywa kwa njia ya mkupuo mara moja tu, kulingana na maelekezo ya Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar.

Fao la kuumia kazini ni miongoni mwa mafao muhimu yanayotolewa na ZSSF kwa lengo la kuwalinda wafanyakazi dhidi ya madhara yatokanayo na kazi.

Uwepo wa fao hili unaonesha dhamira ya Serikali Zanzibar katika kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanapata hifadhi ya kijamii wanapopatwa na majanga yanayotokana na kazi.

Ni muhimu kwa waajiri na wafanyakazi kuelewa haki, wajibu na taratibu zinazohusiana na fao hili ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanaostahili wanapata huduma hiyo kwa wakati na kwa mujibu wa sheria.

**Usikose Makala ijayo itakayozungumzia Mafao Mengine, utaratibu wa kupata Mafao hayo na nani anastahili kupata mafao hayo.**



# Wananchi Pemba waishukuru Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kuwapatia elimu ya sheria



*Mratibu wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba, Ndg. Massoud Nassor Mohammed akiwasilisha mada kuhusu migogoro ya ardhi kwa wananchi wa Shehia ya Vitongoji na Kibokoni, Mkoa wa Kusini Pemba.*



*Bi Zaituni Hamad mkaazi wa Shehia ya Vitongoji Mkoa wa Kusini Pemba, akichangia mada wakati Watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu walipotembelea shehia yao na kutoa elimu ya sheria.*



*Bw. Faiz Khamis, mkaazi wa Vitongoji Mkoa wa Kusini Pemba, akitoa maoni yake wakati Watendaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu walipotembelea katika shehia ya Vitongoji kutoa elimu ya sheria.*

**NA MWANDISHI WETU**

WANANCHI wa Shehia ya Vitongoji na Kibokoni Kisiwani Pemba wameishukuru Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa kuwapa elimu ya kisheria, kwani hawakuwa na ufahamu wa kutosha wa mambo mambalimbali ya kisheria.

Wakizungumza hayo wakati Mawakili wa Afisi hiyo walipokwenda kutoa elimu kwa wananchi hao, ambapo walisema Afisi hiyo imewafikia katika wakati muafaka hasa ikizingatiwa kuwa wengi wao hawajui kutofautisha kati ya makosa ya jinai na mashauri ya madai.

Sheha wa Shehia ya Vitongoji, Bw. Salim Ayoub Suleiman alisema, "Wengi wetu hatujui kutofautisha makosa ndio maana watu wanaingia katika hatia kwa kukosa tu uelewa wa sheria".

Miongoni mwa mambo waliyolalamikia kutokuwa na uelewa ni pamoja na taratibu za ukamataji wa Polisi kwa watuhumiwa na sheria ya udhalilishaji waliyodai inawatia wanaume wengi hatiani kuliko wanawake.

Aidha walilalamikia Mahkama ya Ardhi kwa kudai kuwa inawapa wasiwasi wa kupata haki wanyonge pale wanapokuwa na kesi za migogoro ya ardhi dhidi ya watu wenye uwezo.

Mzee Omar Mjaka, mkaazi wa Vitongoji aliwashukuru Mawakili hao kwa kufika katika Shehia yao na kufahamu hali halisi ya matatizo yanayowakabili ikiwemo migogoro ya ardhi, mazingira na maamuzi ya kimahkama ambayo alidai hayawafurahishi.

Akizungumza wakati wa kuwasilisha mada kuhusu migogoro ya ardhi, Mratibu wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba, Ndg. Massoud Nassor Mohammed, alisema migogoro hiyo ya ardhi imekithiri katika maeneo mbalimbali kutokana rasilimali hiyo kupanda thamani.

Mbali na hilo, aliwaomba wananchi hao pale wanapowaazima wenzao mashamba kwa ajili ya kilimo, wasiwaruhusu kupanda miti ya kudumu ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza.

Kwa upande wake Wakili wa Serikali, Ndg. Safia Sultan akiwasilisha mada ya ukomo wa madai, alisema migogoro ipo mingi katika jamii hivyo





kuna haja ya kujua taratibu za kufungua mashauri ya madai ili kupata haki.

"Kesi zote za madai zinazo muda wake maalum wa kuzifungua Mahkamani, hivyo watu wasibweteke kufungua kesi muda wanaotaka wao, ni kosa na kunaweza kumkosesha mtu haki zake", alisema Wakili huyo.

Akitoa mfano wa sheria ya ukomo wa masuala ya madai, alieleza kuwa, ukomo wa mtu kufungua dai mahkamani ni miaka 12 na ikitokea mtu kufungua dai baada ya miaka 12, dai hilo ni batili kwani sheria ya ukomo inamzuia.

Aidha alieleza kuwa madai mengine kama ya Pesa, kusababishiana madhara, kubadilisha matumizi ya bidhaa au vifaa, kuvunja mkataba na madai ya mishahara, yote yana ukomo maalum wa muda. Hivyo, amesisitiza jamii kupata elimu.

Kuhusu suala mabadiliko Wakili Jecha Vuai, alisema hilo ni suala mtambuka ambalo litahitaji kuzungumzwa pale watu wanapokutana kutokana na umuhimu wake.

Aidha Wakili Jecha aliwaomba wananchi kisiwani Pemba kufika Afisi ya Mwanasheria Mkuu huko Chake Chake kwa lengo la kujifunza sheria ili kujua haki na wajibu wao.

Afisi ya Mwanasheria Mkuu miongoni mwa majukumu yake ni kutoa elimu kwa jamii ambapo imejipangia utaratibu wa kufika katika shehia za mijini na vijijini kwa lengo la kuwajengea wananchi uwezo wa kisheria ili kuwasaidia kuepuka kuingia katika makosa ya kisheria.



*Mratibu wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba, Ndg. Massoud Nassor Mohammed akimsikiliza mmoja kati ya Wananchi wa Shehia ya Vitongoji wakati Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilipofika Kijijini hapo kutoa elimu ya kisheria.*

# Maswali na Majibu: Kuelewa Kazi za Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

## 1. Kazi ya Ushauri wa Kisheria

***Swali: Kwa nini ushauri wa kisheria ni muhimu katika maamuzi ya Serikali?***

**Jibu:** Ushauri wa kisheria unasaidia kuhakikisha kuwa sera, maamuzi na hatua za Serikali zinaendana na katiba na sheria za nchi. Hivyo, kupunguza uwezekano wa kutokea migogoro, ubatilifu wa maamuzi au hasara za kifedha.

---

***Swali: Nani hunufaika na ushauri wa kisheria kutoka Afisini?***

**Jibu:** Wizara, Idara, Taasisi, Mashirika ya Umma pamoja na Umma kwa ujumla hutegemea ushauri wa kisheria katika maamuzi yao na hivyo kuongoza vyema utekelezaji wa majukumu yao.

## 2. Uwakilishi katika Mashauri ya Madai

***Swali: Ni nani huiwakilisha Serikali Mahakamani katika mashauri ya madai?***

**Jibu:** Wawakilishi wa Serikali Mahakamani katika mashauri ya madai ni Wanasheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, wanaofahamika kitaalamu kama ni Mawakili wa Serikali.

---

***Swali: Kwa nini uwakilishi wa Mawakili wa Serikali ni muhimu?***

**Jibu:** Uwakilishi wa Mawakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria mkuu Zanzibar ni muhimu sana kwasababu Afisi hii ndio msimamizi mkuu wa masuala ya kisheria ya Serikali.

.

---

***Swali: Kuna umuhimu gani wa mashauri ya Serikali kusimamiwa na Mawakili wa Serikali?***

**Jibu:** Katika kusimamia mashauri ya Serikali, Mawakili wa Serikali wanasaidia kulinda maslahi ya Umma, kuratibu mashauri ya Serikali, kuimarisha uwajibikaji na weledi, kuepusha migongamano ya kisheria, na kuokoa gharama za kifedha kwa Serikali.

## 3. Umuhimu wa Kuzingatia Sheria Katika Utungaji wa Sheria

***Swali: Afisi inasaidia vipi kuhakikisha uzingatiaji wa sheria?***

**Jibu:** Kabla ya sheria yoyote kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi, Afisi inasaidia kuhakikisha kuwa mswada umepitiwa na kuchambuliwa ili mswada uendane na matakwa ya kikatiba, kisheria na vigezo vya uandishi wa kisheria.

---

***Swali: Nini hutokea ikiwa taratibu hazijazingatiwa katika utungaji wa sheria?***

**Jibu:** Iwapo taratibu hazijazingatiwa katika utungaji wa sheria, hali hii inaweza kusababisha Serikali kufunguliwa mashauri Mahakamani au kubatilishwa kwa maamuzi ya Serikali.





# Maswali na Majibu

## 4. Uandishi na Uhakiki wa Mikataba

***Swali: Kwa nini mikataba ya Serikali hupaswa kuhakikiwa na Afisi?***

**Jibu:** Mikataba ya Serikali inapaswa kuhakikiwa na Afisi ili kuhakikisha kuwa kabla ya mikataba kusainiwa, maslahi ya Serikali yamezingatiwa kwa lengo la kupunguza migongano ya kisheria.

---

***Swali: Ni hatari zipi hupunguzwa?***

**Jibu:** Katika kufanya uhakiki wa mikataba, Afisi inasaidia kupunguza hasara za kifedha, masharti yasiyotekelezeka, mikataba isiyotekelezeka na migogoro isiyoisha.

## 5. Uandishi wa Sheria

***Swali: Afisi ina jukumu gani katika utungaji wa sheria?***

**Jibu:** Afisi ina wajibu wa kuandaa miswada, kanuni ndogo na kupitia maandiko ya kisheria ili kuhakikisha uwazi, ulinganifu na uhalali wake kikatiba.

---

***Swali: Kwa nini uandishi mzuri wa sheria ni muhimu?***

**Jibu:** Sheria zilizoandikwa vizuri zinaweza kuondoa utata, mianya na changamoto za utekelezaji.

## 6. Masuala ya Kisheria ya Kikanda na Kimataifa

***Swali: Afisi ina jukumu gani katika masuala ya kikanda na kimataifa?***

**Jibu:** Katika masuala ya kikanda na kimataifa, Afisi inatoa ushauri kuhusu mikataba na makubaliano ya kikanda na kimataifa yanayohusisha Serikali.

---

***Swali: Kwa nini uchambuzi wa kisheria ni muhimu kwa mikataba ya kikanda na kimataifa?***

**Jibu:** Afisi inafanya uchambuzi wa kisheria kwa mikataba ya kikanda na kimataifa ili kuhakikisha makubaliano yoyote yanayohusisha nchi yako halali na yana maslahi kwa taifa.

## 7. Mapitio na Utafiti wa Sheria

***Swali: Ni nini tofauti ya mapitio na utafiti wa sheria?***

**Jibu:** Mapitio ya sheria hufanyika kwa sheria ambazo tayari zimeshatungwa kisheria na zinaendelea kufanyiwa kazi. Kwa upande wa utafiti wa sheria, ni kazi ambayo inafanyika kwa eneo ambalo halina kabisa sheria.

---

***Swali: Kwa nini ni muhimu kufanya mapitio na utafiti wa sheria?***

**Jibu:** Mapitio na utafiti wa sheria unasaidia kubaini mapungufu ya kisheria na kufahamu uhalisia wa kurekebisha sheria au kutunga sheria mpya.



# Tunataka ubingwa michuano ijayo ya Mei Mosi – Kocha Abdulshakur

**NA MWANDISHI WETU**

Kocha wa timu ya mpira wa miguu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu Ndg. Abdulshakur Abdalla, amesema bado ana imani kubwa na kikosi hicho licha ya kutolewa katika hatua ya robo fainali kwenye michuano ya Mei Mosi mwaka 2026.

Akizungumza na Jarida hili wakati akitoa tathmini ya michuano ya Mei Mosi 2026, Kocha huyo ambaye ni Wakili wa Serikali katika Afisi hiyo alisema pamoja na kutolewa kwenye hatua hiyo, kikosi hicho kimeonesha uwezo mkubwa.

Alisema katika hatua ya makundi, timu hiyo iliibugiza Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa mabao 7-1 na baadae kuishushia kipigo kikali cha magoli 5-1 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Aidha, Timu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliifunga timu ya Chuo cha Mwalimu Nyerere mabao 7-4 kabla ya kufungwa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) magoli 2-1.

"Kimsingi timu yetu ilikuwa bora ndio maana tulizifunga mabao mengi timu tulizokutana nazo katika hatua ya makundi kabla ya kupoteza 1-0 katika hatua ya robo fainali", alisema Abdulshakur.

Alisema kutokana na matokeo hayo timu hiyo inauwezo na kila sababu ya kubeba ubingwa kwenye michuano ya mwakani.

Akizungumzia kuhusu maendeleo ya michezo kwa ujumla wake, Kocha



huyo aliishauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuandaa uongozi utakaoratibu michezo yote ikiwemo mpira wa miguu, mpira wa kikapu, tenis na riadha.

Alisema ni vyema watendaji wa Afisi kuwa imara muda wote kwa kufanya mazoezi hata kipindi ambacho hakuna mashindano hatua ambayo itaimarisha afya zao na kuleta ufanisi katika utendaji wa majukumu yao.

“Michezo ni afya na kujitangaza, tunapaswa kuwa na timu imara ya muda wote na kwenda sehemu tofauti mijini na vijijini kwa ajili ya michezo ya kirafiki”, alifahamisha Kocha Abdulshakur.


Awali, Kocha huyo aliupongeza uongozi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mashirikiano makubwa waliyoipa timu ya Soka ya Afisi hiyo hasa kwa kuwapatia motisha wachezaji walipokuwa katika mashindano.


Katika mechi ya mwisho ya robo fainali timu ya soka ya Afisi Mwanasheria Mkuu ilikubali kwa tabu kichapo cha 1-0 dhidi ya timu ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

***Kocha wa timu ya soka ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Ndg. Abdulshakur Abdalla akizungumza na wachezaji wa Timu hiyo wakati wa mapumziko katika mchezo ulioikutanisha timu hiyo dhidi ya Timu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.***



# Kibonzo...


SHAMBA HILI NI LANGU
HAPANA SIYO LAKO NI LANGU
KAMA NI LAKO, JE! UNA USHAHIDI GANI?
HATI HALALI KUTOKA KAMISHENI YA ARDHI HII HAPA!! TULIA MZEE HILI SHAMBA NI LANGU.


TUZIJUE SHERIA ZA ARDHI ILI KULINDA MALI ZETU KIHALALI NA KUEPUKA MIGOGORO.
WANANCHI WAKIPEWA ELIMU NA MWANASHERIA JUU YA UMUHIMU WA KUZIJUA SHERIA ZA ARDHI ILI KULINDA MALI ZAO KIHALALI NA KUEPUSHA MIGOGORO YA MIPAKA YA ARDHI.

# Nasaha za Mshairi

## SHAIRI: TUTUNZE MIUNDO MBINU
## NA HAMAD ALI KOMBO (DKT. MSHIKO)

1 Tunaiona nchini  Miundo mbinu yang'ara
Njia hadi chochoroni  Zimesadifu imara
Twataka tupewe nini  Semeni hebu jahara
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

2 Kusi na kaskazini  Kwa macho tunaiona
Nuru ya matumaini Tayari imeshapwana
Sasa tuzitumieni  Fursa kila aina
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

3 Nikingia sukulini  Mambo huko metawala
Majengo ya maroshani Yajengwa kila mahala
Watoto wa darasani  Wanasoma kwa muwala
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

4 Wote wakaa vitini   Msingi na sekondari
Vilopangika makini   Vizuri kwa mstari
Mepata matumaini  Kwakweli hili twakiri
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

5 Mwenye macho wazamani  Wesema kwa yao nia
Kila aliyena mboni  Simwambie angalia
Nahili naliamini  Kwa huko tunoendea
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

6 Nikigeuka sokoni   Nako mambo yamekuwa
Yamejengwa yaroshani  Mazuri yakuvutia
Raia wote nchini  Kwakweli wafurahia
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

7 Sasa kilo baki kwetu  Vyema kuisimamia
Kuilinda tuthubutu  Isijekuharibiwa
Isije ikawa butu   Lengo hatutafikia
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

8 Tuidumishe amani  Mambo yazidi vutia
Utulivu wa nchini  Tuzifuate sheria
Sheria zilo makini  Tusijekuzipindua
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

9 Miundo mbinu ni tija  Ikiwa tutaitunza
Huwa kwetu ni daraja  Kutuvuusha laweza
Hivyo basi ipo haja  Kamba tusijelegeza
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

10 Tuliambiwa kangaja  Wakale walieleza
Mambo huenda yakaja   Nasasa yashachomoza
Tusivifanye vioja   Kuvuruga tukaanza
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**

11 Tuitunze iwe vyema  Wambali waitumie
Iunufaishe uma    Wala isihujumiwe
Watanufaika jama   Wajao wahadithie
**Tutunze miundo mbinu   Idumu dumu dawamu**

12 Tutunze ili idumu  Idumu dumu dawama
Idumu iwe timamu   Hadi karne nzima
Atakae ihujumu   Sheria kumuandama
**Tutunze miundo mbinu  Idumu dumu dawamu**



AGC ZANZIBAR | ATTORNEY-GENERAL'S CHAMBERS

# Attorney General's Chambers










**Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar,**
**S.L.P. 259, Mazizini, Zanzibar, Tanzania. Simu: +255 22 233455**
**barua pepe: agcsmz@agcz.go.tz | www.agcz.go.tz**
**Afisi_ya_mwanasheriamkuu_znz**